# SERA YA HABARI NA UTANGAZAJI

## UTANGULIZI

Sekta ya Habari na Utangazaji ni moja ya sekta za huduma za jamii nchini. Sekta hii inatoa huduma ambayo ni haki ya msingi ya raia kama inavyotamkwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Ibara ya 18 ya Katiba inasema:

(1) Kila mtu yuko huru kuwa na maoni yoyote na kutoa nje mawazo yake, na kutafuta, kupokea na kutoa habari na dhana zozote kupitia chombo chochote bila ya kujali mipaka ya nchi, na pia ana uhuru wa mawasiliano yake kutoingiliwa kati.

(2) Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbali mbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii.

Aidha, kutoa na kupokea habari kunatambuliwa duniani kote kuwa ni moja ya haki za binadamu. Umoja wa Mataifa, na Umoja wa Afrika zina matamko rasmi ambayo serikali imeridhia kuhusu haki ya kupokea na kutoa habari. Haki hii, kama zilivyo haki nyingine zote, hutolewa kwa kuzingatia wajibu wa kila raia kwa jamii na uhuru binafsi wa binadamu.

Dhima ya Sekta ya Habari na Utangazaji katika jamii ni kutoa habari, kuelimisha na kuburudisha. Sekta hii inahudumiwa na vyombo vya habari ambavyo ni redio, magazeti, majarida, televisheni, filamu, video, intaneti, picha, vipeperushi, katuni na mabango. Maendeleo ya teknolojia ya mawasiliano yamerahisisha upataji na utoaji habari.

Sekta hii imekua sana tokea Sera ya Habari na Utangazaji ilipotolewa mara ya kwanza mwaka 1993. Idadi ya magazeti ya kila siku imeongezeka kutoka mawili (2) mwaka 1992 hadi kumi na mbili (12) Januari, 2003. Aidha, idadi ya magazeti ya kila wiki imeongezeka kutoka matano mwaka 1992 hadi 30 mwezi Januari, 2003. Kadhalika idadi ya vituo vya redio Tanzania Bara imeongezeka kutoka kimoja mwaka 1992 hadi 30 mwezi Januari, 2003. Tanzania Bara hivi sasa ina vituo vya televisheni zaidi ya 30 ikiwemo Televisheni ya Taifa (TVT) iliyoanzishwa mwaka 2000. Wakati Sera inatolewa mwaka 1993, kulikuwa hakuna hata kituo kimoja. Aidha, idadi ya vyuo vya uandishi wa habari imeongezeka kutoka viwili mwaka 1993 hadi vinane mwezi Januari, 2003. Viwili kati ya vyuo hivyo ni vyuo vikuu. Vilevile, Tume ya Utangazaji Tanzania ilianzishwa mwaka 1993 kusimamia Sekta ya Utangazaji na baadaye, mwaka 2003, iliunganishwa na Tume ya Mawasiliano kuanzisha Tume ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Asilimia kubwa ya magazeti na machapisho mengine husomwa zaidi mijini ambako usambazaji ni rahisi, na kiwango cha kujua kusoma na kuandika ni kikubwa.

Baadhi ya Serikali za Mitaa na Halmashauri za Wilaya na Miji zimeanzisha vituo vya televisheni ambavyo hugharamiwa na halmashauri hizo.

Aidha yapo magazeti na majarida yatolewayo na Asasi Zisizokuwa za Kiserikali na mashirika ya dini, ambayo mara nyingi hugharamia vyombo vyao vya habari.

Intaneti imeanza kuingia kwa nguvu nchini, na miji mingi sasa ina huduma hiyo. Hadi Desemba, 2002, kulikuwa na makampuni 21 ya huduma za intaneti (Dar es Salaam 19, Arusha 1 na Mwanza 1).
Idara za serikali, mashirika, na asasi za aina zote zinajitahidi kuwa na tovuti zao, ili wananchi wapate habari za vyombo hivyo kupitia mtandao huo wa kompyuta.

Tasnia ya habari ina vyama vya aina nyingi vilivyoundwa na wanahabari wenyewe. Kuna vyama vya kitaaluma, vyama vya kutetea maslahi na hali bora, kulinda maadili na uhuru wa vyombo vya habari, vyama vya kuendeleza maslahi ya wanahabari wanawake na kadhalika. Aidha, zipo klabu za waandishi wa habari katika mikoa mingi. Hadi kufikia Desemba, 2002 mikoa 18 ilikuwa na klabu za waandishi wa habari, ambazo, licha ya kuratibu masuala ya taaluma ya habari katika mikoa, pia zinachangia katika kuhamasisha maendeleo ya wananchi.

Serikali ina Idara ya Habari (MAELEZO), ambayo wajibu wake umeainishwa katika Kanuni ya Kudumu C.16, na Sheria iliyofuta SHIHATA Na. 7 ya Mwaka 2000. Idara hii ina ofisi katika baadhi ya mikoa ya Tanzania Bara. Aidha, Wizara zote zimeteua maofisa watakaoshughulikia habari, elimu na mawasiliano. Kuwepo kwa maofisa hao katika wizara na asasi, mashirika na makampuni mbalimbali huleta uhusiano mzuri kati ya watoaji na watumiaji wa huduma hizo.

Pamoja na maendeleo yaliyopatikana katika Sekta ya Habari na Utangazaji, utoaji wa huduma katika sekta umekuwa si wa kuridhisha kutokana na sababu mbalimbali ambazo ni pamoja na:

- Sera ya mwaka 1993 kutoeleza kwa ufasaha nafasi ya Sekta ya Habari na Utangazaji katika maendeleo ya taifa kwa jumla. Matokeo yake ni kwamba bado kuna baadhi ya watu wenye mtazamo wa kuona chombo cha habari kuwa nyenzo ya kufanikisha malengo yao binafsi badala ya yale ya utoaji huduma kwa jamii. Aidha, baadhi ya wamiliki wa vyombo vya habari wamekuwa wakijali zaidi kupata faida bila kuzingatia maslahi ya taifa.

- Baadhi ya vipengele vya Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 na Sheria ya Utangazaji ya Mwaka 1993 vina upungufu mkubwa ambao umesababisha malalamiko mengi.

- Kuna malalamiko mengi dhidi ya maelekezo kwamba vituo binafsi vya redio na televisheni vitangaze katika eneo lisilozidi asilimia 25 ya nchi. Serikali ilitoa maelekezo hayo mwaka 1994 kwa mujibu wa Sheria ya Utangazaji Na.6 ya Mwaka 1993 kwa lengo la kulinda maslahi ya Taifa kutokana na uchanga wa tasnia ya utangazaji binafsi hapa nchini. Baada ya miaka 10 ya utangazaji binafsi na kutokana na maendeleo makubwa ya teknolojia ya habari na mawasiliano, serikali imeshauriwa kuangalia upya maelekezo hayo.

- Hivyo, madhumuni ya kuwa na Sera Mpya ya Habari na Utangazaji ni kuondoa mapungufu yaliyojitokeza ili sera hiyo iendane na mazingira mapya ya kisiasa, mabadiliko ya kiuchumi na maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano duniani.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 DIRA NA MALENGO YA SERA YA HABARI NA UTANGAZAJI

### 1.1 Dira ya Sera

Dira ya sera hii ni kuwepo kwa vyombo vingi vya habari, vinavyomilikiwa na umma na sekta binafsi, na vilivyo imara na anuwai, na vinavyozingatia maadili ya taaluma na ya jamii, ili viweze kuchangia katika kufanikisha malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.

Aidha, dira ya sera hii mpya inahimiza kuwepo kwa taasisi za mafunzo, utafiti na ushauri wa kitaalam kwa lengo la kuboresha tasnia ya habari na zinazochangia kukuza sekta ya filamu na video, kwa minajili ya kuibua na kukuza vipaji na kulinda historia na utamaduni wa Tanzania.

Sera pia inaelekeza kuwepo kwa vyombo vya habari vilivyosambaa nchi nzima.

### 1.2 Malengo/Madhumuni ya Sera

Madhumuni na Malengo ya Sera ya Habari na Utangazaji ni kama yafuatayo:

- Kuweka mazingira yanayowezesha ukuaji wa Sekta ya Habari na Utangazaji nchini kote;

- Kuhamasisha vyombo vya habari kutoa huduma kwa kuzingatia maadili ya taaluma na maadili ya jamii;

- Kuhamasisha wanahabari kuanzisha na kuendeleza chombo cha kusimamia maadili ya taaluma ya Habari na Utangazaji;

- Kuweka utaratibu wa kujenga uwezo endelevu katika sekta.

## SURA YA PILI

## 2.0 MALENGO NA MATAMKO YA SERA

### 2.1.0 HAKI, UHURU NA WAJIBU WA VYOMBO VYA HABARI

Hivi sasa upatikanaji wa haki ya kikatiba ya uhuru wa kutoa na kupokea habari unategemea sheria ambazo zinalalamikiwa kuwa zinaondoa haki hiyo, kwa mfano Sheria ya Usalama wa Taifa Na. 3 ya Mwaka 1970, Sheria ya Magazeti Na. 7 ya Mwaka 1976, Sheria ya Utangazaji Na. 6 ya Mwaka 1993 na sheria nyinginezo zinazohusiana na Sekta ya Habari na Utangazaji. Aidha, vyombo vya habari vya Serikali na binafsi haviwafikii wananchi wote kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali na sheria na kanuni zilizopo. Vilevile, kuna ukosefu wa miundombinu ya mawasiliano na uelewa mdogo wa dhana ya uhuru na wajibu wa vyombo vya habari miongoni mwa wamiliki, watendaji wa vyombo hivyo na wananchi.

### 2.1.1 Malengo ya Sera

- Kuondoa vikwazo vinavyokwamisha upatikanaji wa haki ya wananchi ya kupokea na kupata habari;
- Kuelimisha wananchi kuhusu haki yao ya kikatiba ya kupata na kutoa habari;
- Kuhamasisha uanzishwaji wa vyombo vya habari nchini kote;
- Kuhamasisha uwekezaji katika miundombinu ya mawasiliano kote nchini;
- Kuhamasisha na kuelimisha wamiliki na watendaji wa vyombo vya habari kuhusu wajibu wa vyombo vya habari kwa jamii.

## 2.2 SHERIA ZA VYOMBO VYA HABARI

Kuna malalamiko kwamba Sheria za magazeti na utangazaji zinampa Waziri mwenye dhamana ya habari na utangazaji mamlaka ya kuadhibu vyombo vya habari ambavyo vinachapisha au kutangaza taarifa ambazo, kwa tafsiri yake Waziri, zinatishia maslahi ya umma.

### 2.2.1 Malengo ya Sera

Kupitia Sheria zinazolalamikiwa ili:

- Kuwezesha wananchi kufaidi kwa ukamilifu haki ya msingi ya kupata na kutoa habari kama ilivyoainishwa katika Katiba ya nchi;

- Kulinda wanahabari wanaotekeleza wajibu wao kwa mujibu wa maadili ya taaluma na ya jamii;

- Kulinda haki, uhuru na wajibu wa vyombo vya habari;

- Kutoa nafasi sawa kwa wawekezaji katika sekta ya habari;

- Kuondoa usiri usio wa lazima.

### 2.2.2 Maelekezo ya Sera

- Serikali itahakikisha sheria za vyombo vya habari zinazolalamikiwa zinadurusiwa na kurekebishwa;

- Serikali itahakikisha kuwa sheria za vyombo vya habari zinazingatia haki ya kusuluhishwa kupitia mkondo wa Mahakama;

- Serikali itasimamia kutungwa kwa sheria moja inayotawala vyombo vya habari.

## 2.3 UMILIKI WA VYOMBO VYA HABARI

Hivi sasa mmiliki mmoja anaruhusiwa kuwa na zaidi ya chombo kimoja cha habari. Aidha, baadhi ya vyombo vya habari vimeanzishwa bila watendaji wenye taaluma. Wamiliki wengine wa vyombo vya habari hawatoi mafunzo kazini kwa watumishi wao. Vilevile, baadhi ya vituo vya redio na televisheni vinatumiwa na wawekezaji na mashirika ya habari ya nje kueneza sera na utamaduni wa mataifa ya nchi za nje na hivyo kuathiri mila na utamaduni wetu. Baadhi ya wawekezaji hao wa nje pia wanadhibiti maudhui ya baadhi ya vyombo vya habari hapa nchini, na hivyo kuathiri mtazamo wa kizalendo wa wananchi.

### 2.3.1 Malengo ya Sera

- Kuendelea kuruhusu mmiliki mmoja kuwa na zaidi ya chombo kimoja cha habari;

- Kuvifanya vyombo vya habari vizingatie wajibu wa kutoa huduma kwa manufaa ya umma;

- Kuhakikisha mmiliki wa chombo cha habari ana watendaji wenye taaluma;

- Kuwahamasisha wamiliki wa vyombo vya habari kuwaendeleza watumishi wao kitaaluma;

- Kuhakikisha kwamba uendeshaji wa vyombo vya habari unakuwa mikononi mwa Watanzania, na wageni wanaajiriwa tu kama utaalam wao haupatikani nchini.

### 2.3.2 Maelekezo ya Sera

- Serikali iendelee kuwaruhusu wamiliki kuwa na zaidi ya chombo kimoja cha habari;

- Raia wa nchi za nje wanaweza kuwekeza katika chombo cha habari kwa ubia na raia, ili mradi hisa za Mtanzania zisiwe chini ya asilimia 51 kumwezesha kuongoza chombo hicho wakati wote;

- Uendeshaji wa vyombo vya habari utakuwa mikononi mwa Watanzania;

- Wageni wataajiriwa tu kama utaalam wao unaohitajika haupatikani nchini;

- Serikali iwahamasishe wawekezaji kuanzisha vyombo vya habari katika maeneo ambayo hayavutii kibiashara;

- Chombo cha habari kisitumiwe kwa manufaa binafsi ya mmiliki au mtendaji, bali kitatumiwa kwa maslahi ya umma;

- Chombo cha habari kiongozwe na maadili ya taaluma na ya jamii husika;

- Chombo cha habari kisitangaze habari kwa misingi ya ubaguzi wa rangi, kabila, dini, jinsia au ulemavu au kuchochea uhasama;

- Lugha zitakazotumiwa na vyombo vya habari hapa nchini ni Kiswahili na Kiingereza.

## 2.4 SERIKALI NA HABARI

Baadhi ya wananchi hivi sasa hawapati huduma ya habari kupitia vyombo vya habari vya Serikali kwa kuwa baadhi ya maeneo ya nchi hayana miundombinu ya mawasiliano. Aidha, dhana ya uwazi na ukweli haitekelezwi ipasavyo kutokana na sheria, kanuni na taratibu za usiri Serikalini. Vilevile kuna migongano ya taarifa zitolewazo na taasisi mbalimbali za Serikali. Kutoshirikishwa kwa Idara ya Habari kama Msemaji Mkuu wa Serikali katika vikao vinavyotoa maamuzi mbalimbali na ukosefu wa watendaji wenye taaluma ya habari katika Wizara, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa hufanya Serikali kushindwa kutoa taarifa za utekelezaji wa majukumu yake kwa ukamilifu kwa wananchi kupitia vyombo vya habari.

### 2.4.1 Malengo ya Sera

- Kuimarisha huduma za vyombo vya habari vya Serikali nchini kote, na hasa katika maeneo yasiyopendelewa na wawekezaji binafsi;

- Kuondoa vikwazo vya upatikanaji wa habari Serikalini na taasisi zake;

- Kuendeleza Idara ya Habari kama Msemaji Mkuu wa Sera za Serikali na Mratibu Mkuu wa Habari kuhusu shughuli za Serikali;

- Kuimarisha vitengo vya habari vya wizara, idara na taasisi za Serikali, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

- Kuweka utaratibu wa Msemaji wa Serikali katika ngazi za wizara, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Taasisi za Serikali;

- Kuimarisha taasisi za Serikali za kutoa mafunzo ya taaluma ya habari.

### 2.4.2 Maelekezo ya Sera

- Serikali iendelee kumiliki vyombo vya habari na kuwekeza katika huduma za habari kote nchini;

- Serikali iendelee kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha vyombo vya habari kote nchini;

- Serikali iondoe vikwazo vinavyozuia upatikanaji wa habari za manufaa kwa wananchi;

- Serikali iendelee kuwa na wasemaji wake katika ngazi za taifa, wizara, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na taasisi za Serikali;

- Serikali iimarishe Idara ya Habari ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

## 2.5 MAGAZETI NA MAJARIDA

Hivi leo, kuna ukiukwaji mkubwa wa maadili ya taaluma ya uandishi wa habari na ya jamii na uanzishwaji holela wa vijarida. Pia asilimia kubwa ya nchi haina huduma ya magazeti na gharama za huduma za magazeti hivi sasa ni kubwa. Aidha, baadhi ya magazeti na majarida yanachapisha taarifa na picha zinazochochea uvunjaji wa maadili kama kuchochea vitendo vya ngono na kadhalika.

### 2.5.1 Malengo ya Sera

- Kuhakikisha magazeti na majarida yanazingatia maadili ya taaluma na maadili ya jamii na kuhakikisha kwamba magazeti na majarida yote yanasajiliwa kwa mujibu wa sheria;

- Kutafuta njia za kupunguza bei za magazeti;

- Kuhimiza uzingatiaji wa maadili ya jamii na ya taaluma ya uandishi wa habari.

### 2.5.2 Maelekezo ya Sera

- Magazeti na majarida yataendelea kusajiliwa na Serikali kwa mujibu wa sheria;

- Serikali itaendelea kuzihamasisha taasisi na asasi mbalimbali kuanzisha magazeti na majarida katika maeneo yao ili kuwe na uwiano mzuri wa upatikanaji wa habari kati ya mijini na vijijini;

- Serikali ihamasishe wamiliki wa kampuni za uchapishaji kushirikiana katika kutafuta njia za kupunguza gharama za uchapishaji;

- Majarida ya burudani na starehe yatasajiliwa kwa mujibu wa sheria, na yatachapishwa na kusambazwa kwa kuzingatia maadili ya Kitanzania na Kanuni zitakazowekwa.

## 2.6 MASHIRIKA YA HABARI

Idara ya Habari ambayo ni moja ya mashirika ya habari, haina rasilimali za kuiwezesha kutekeleza kikamilifu majukumu ya kihabari yaliyoachwa na Shirika la Habari Tanzania (SHIHATA). Aidha kuna uwekezaji mdogo kwenye mashirika ya habari na pia kuna ukosefu wa miundombinu ya mawasiliano ya habari katika maeneo mengi ya vijijini.

### 2.6.1 Malengo ya Sera

- Kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza kwenye mashirika ya habari;

- Kuwezesha Idara ya Habari kuwa na nyenzo na watalaam wa kutosha kuweza kutekeleza majukumu yake;

- Kuhamasisha uwekezaji kwenye miundombinu ya mawasiliano ya habari.

### 2.6.2 Maelekezo ya Sera

- Serikali iimarishe Idara ya Habari ili itekeleze majukumu yake kwa kuipatia wataalam, vitendea kazi, na nyenzo nyingine;

- Sekta binafsi ihamasishwe kuwekeza kwenye mashirika ya habari;

- Serikali ihamasishe na kushirikisha sekta binafsi kuwekeza kwenye miundombinu ya habari na mawasiliano.

## 2.7 REDIO, TELEVISHENI NA INTANETI

- Hivi sasa intaneti haitawaliwi na sheria yoyote nchini, baadhi ya vipindi vya redio na televisheni havizingatii maadili ya Kitanzania, maeneo mengi ya vijijini hayana huduma ya televisheni na vituo vingi vya utangazaji vina vipindi vichache vyenye maudhui ya Kitanzania kwa kuwa watumishi wengi wa vituo hivyo hawana taaluma ya kutosha. Vilevile hakuna utaratibu maalum kwa vituo binafsi vya redio na televisheni kujiunga na vituo vya Serikali katika kutangaza matukio maalum ya kitaifa.

### 2.7.2 Malengo ya Sera

- Kuweka huduma za intaneti chini ya sheria na taratibu zinazotawala huduma za redio na televisheni;
- Kuhakikisha kuwa maudhui ya vipindi vya redio na televisheni yanazingatia maadili ya taaluma na ya jamii;
- Kuhamasisha kuanzishwa kwa huduma ya televisheni maeneo ya vijijini;
- Kuhamasisha vituo vya redio na televisheni kuajiri watumishi wenye taaluma ya habari na utangazaji;
- Kuweka utaratibu wa vituo binafsi ya redio na televisheni kujiunga na redio na Televisheni ya Taifa kutangaza matukio maalum ya kitaifa.

### 2.7.3 Maelekezo ya Sera

- Redio, televisheni na intaneti ziendelee kusajiliwa kwa mujibu wa sheria;

- Vituo vya redio na televisheni na intaneti vitatakiwa kuzingatia maadili ya taaluma na ya jamii na utamaduni wa Tanzania;

- Redio na televisheni za binafsi zitangaze katika eneo lolote la nchi kwa mujibu wa kanuni na taratibu za utangazaji zitakazowekwa na mamlaka za usimamizi wa utangazaji;

- Maudhui ya vipindi vya redio na televisheni yaimarishe amani, umoja, mshikamano na usalama wa taifa;

- Vituo vya redio na televisheni vizingatie athari za matumizi ya vipindi vya nje kwa utamaduni na maadili ya Taifa;

- Lugha za kurushia matangazo ya redio na televisheni nchini ni Kiswahili na Kiingereza;

- Redio na televisheni binafsi zishiriki kikamilifu katika ujenzi wa Taifa na katika kampeni za taifa na maafa;

- Vituo vya intaneti vijitahidi kuwaepusha watoto na athari mbaya za intaneti;

- Utoaji wa masafa ya kutangazia uzingatie vigezo vitakavyowekwa na mamlaka ya usimamizi wa utangazaji;

- Serikali iweke utaratibu wa vituo binafsi vya redio na televisheni kujiunga na redio na Televisheni ya Taifa kutangaza matukio maalum ya Kitaifa.

## 2.8 **FILAMU, VIELELEZO NA VIDEO**

Baadhi ya filamu, video na vielelezo vilivyopo vinachochea vitendo vya ngono na baadhi ya filamu, video na vielelezo vinachochea ubaguzi kwa misingi yakabila, jinsia na dini na pia baadhi ya filamu, video na vielelezo vinachochea fujo, utumiaji wa madawa ya kulevya na unyanyasaji wa jinsia.

### 2.8.1 Malengo ya Sera

- Kuhakikisha kuwa uonyeshaji wa filamu, vielelezo na video unazingatia maadili ya taaluma ya habari na ya jamii;
- Kuhamasisha utengenezaji wa filamu, video na vielelezo vyenye maudhui ya Kitanzania;
- Kukuza vipaji vya wananchi katika fani za filamu, video na vielelezo;
- Kuhamasisha uwekezaji katika tasnia ya filamu, video na vielelezo.

### 2.8.2 Maelekezo ya Sera

- Wamiliki na waendeshaji wa shughuli za filamu, video na vielelezo wasieneze ubaguzi wowote, uchochezi wa kisiasa na kidini au udhalilishaji wa kikundi chochote cha jamii ya Watanzania. Aidha, wahakikishe kuwa silka, maadili, utamaduni na utu wa Mtanzania vinadumishwa na kuheshimiwa;
- Asasi zinazotengeneza filamu, video na vielelezo, ziendeleze vipaji vya Watanzania katika fani mbalimbali na kudumisha utamaduni wao;
- Mamlaka zinazohusika, zisimamie kwa ukamilifu utekelezaji wa sheria zinazotawala maonyesho filamu, video na vielelezo;

- Sanaa na taaluma ya filamu, video na vielelezo iendelezwe.

## 2.9 KUJENGA UWEZO WA SEKTA

Wanahabari wengi hawana mafunzo ya taaluma kwa kuwa kuna vyuo vikuu vichache vinavyotoa taaluma ya habari na ambavyo havikidhi mahitaji ya taifa. Aidha, vyuo vingi vya watu binafsi havina makazi ya kudumu, havina mitaala, havina vifaa vya kufundishia vya kutosha na havina walimu wenye elimu ya juu na uzoefu wa kutosha. Hivyo, mafunzo yatolewayo na baadhi ya taasisi za habari ni ya ngazi ya chini kiasi kwamba hayafikii kiwango cha taaluma kinachotakiwa. Pia, kutokana na utata wa sheria uliopo vyuo vya binafsi vya kufundisha wanahabari vimeanzishwa kama kampuni za biashara.

### 2.9.1 Malengo ya Sera

- Kuwezesha sekta ya habari kuwa na taasisi imara za mafunzo na utafiti;

- Kuinua viwango vya taaluma vya wanahabari;

- Kuwezesha vyombo vya habari kuwa na watendaji wengi na bora ili kukidhi mahitaji ya soko;

- Kuwezesha kupatikana kwa watendaji wenye ujuzi na mbinu za kumudu ushindani kutoka vyombo vya habari vya nje ya nchi;

- Kudumisha uzingatiaji wa maadili ya taaluma na ya jamii.

### 2.9.2 Maelekezo ya Sera

- Mafunzo ya wanahabari yalenge katika ngazi ya elimu ya juu;

- Vyuo Vikuu vya Serikali vianzishe mafunzo ya taaluma yatakayotosheleza fani zote za sekta ya habari na utangazaji;

- Taasisi za mafunzo ya taaluma ya habari na utangazaji zitilie mkazo elimu ya utafiti itakayosaidia kutatua matatizo ya maendeleo ya sekta ya habari;

- Mafunzo ya taaluma ya habari yatolewe na vyuo na taasisi zilizoidhinishwa na vyombo vya usimamizi wa Elimu ya Ufundi na Elimu ya Juu;

- Mafunzo kazini yawe ni haki ya mwanahabari. Mafunzo hayo yalenge kuinua kiwango cha elimu na ujuzi, kuongeza upeo wa masuala ya kijamii na kupata elimu ya teknolojia mpya.

## SURA YA TATU

## 3.0 MGAWANYO WA MAJUKUMU

Katika utekelezaji wa Sera ya Habari na Utangazaji, Serikali na asasi mbalimbali zitatekeleza majukumu yafuatayo:

### 3.1 Serikali

- Kulinda haki ya msingi ya mwananchi ya kupata habari iliyotajwa katika Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) na Ibara ya 19 ya Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu;

- Kuweka mazingira yatakayowezesha kuimarika kwa Sekta ya Habari na Utangazaji;

- Kuratibu, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa Sera.

### 3.2 Baraza la Habari

- Litaimarisha, litadumisha na kuendeleza maadili na viwango vya utendaji katika vyombo vya habari na utangazaji;

- Litashirikiana na wadau katika kukuza haki, uhuru na wajibu wa vyombo vya habari;

- Litaleta uhusiano mwema baina ya wananchi na vyombo vya habari, na baina ya vyombo vyenyewe.

### 3.3 Vyama vya Wanahabari

- Vitasaidia wanachama kupata taaluma katika fani zao;
- Vitainua kiwango cha ufanisi na utendaji katika Sekta ya Habari;
- Vitahamasisha maelewano baina ya wanahabari na vyanzo vya habari;
- Vitaelimisha jamii kuhusu haki yao ya kupata habari;
- Vitatetea maslahi ya wanachama wao.

### 3.4 Vyombo vya habari

- Vitatoa huduma za habari, elimu na burudani kwa kuzingatia maadili na utamaduni wa Mtanzania;
- Vitachangia kuinusuru jamii kutokana na majanga kama vile vita, njaa, magonjwa ya milipuko na uharibifu wa mazingira;
- Vitashiriki katika kampeni za kuendeleza jamii katika nyanja mbalimbali, kama vile kuleta usawa wa jinsia, kupunguza umaskini, kupiga vita rushwa, kuondoa maradhi na ujinga n.k.

### 3.5 Taasisi za Mafunzo

- Zitajenga uwezo wa wanahabari kwa kutoa mafunzo ya fani za habari na utangazaji kulingana na mahitaji ya Sekta ya Habari na Utangazaji;
- Zitafanya utafiti wa masuala mbalimbali kwa madhumuni ya kuendeleza Sekta ya Habari na Utangazaji.

### 3.6 Wamiliki wa vyombo

- Watahakikisha vipindi havikiuki maadili;

- Wataandaa programu za mafunzo.

## 3.7 Vyombo vya Usimamizi

Usimamizi wa Sekta ya Habari na Utangazaji unafanywa na Serikali kupitia Mamlaka mbalimbali za usimamizi wa vyombo vya habari na utangazaji.

- Mamlaka hizo za Serikali zitasimamia utekelezaji wa Sheria ya vyombo vya habari na utangazaji na kuratibu vyombo hivyo ili kuvisaidia viimarike na viendelee kuwahudumia wananchi. Aidha serikali itaendelea kusimamia siyo tu uhuru bali pia uwajibikaji wa vyombo hivyo vya habari kwa jamii kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na maadili ya jamii na ya taaluma ya habari;

- Baraza la Habari litaendelea kulinda haki za watumiaji na watoaji wa huduma ya habari; na kusuluhisha malalamiko yanayotolewa dhidi ya vyombo vya habari na malalamiko ya wanahabari dhidi ya vyanzo vya habari, taasisi na wanajamii wengine. Aidha, litatoa elimu ya umma kuhusu umuhimu,haki na wajibu wa vyombo vya habari, litaendelea kuhimiza vyombo vya habari kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na maadili ya jamii na ya taaluma ya habari, na litaipa Serikali ushauri wa kitaalam kuhusu namna ya kuboresha mazingira ya sekta ya habari.

## SURA YA NNE

# 4.0 URATIBU NA UFUATILIAJI

## 4.1 Uratibu

Idara ya Habari ndiyo mratibu wa masuala yote yanayohusu habari na utangazaji hapa nchini. Ni jukumu la Idara ya Habari kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa Sera hii utakaokuwa unafanywa na vyombo mbalimbali.

## 4.2 Vigezo vya tathmini

Kufanikiwa kwa Sera Mpya ya Habari na Utangazaji kutapimwa kutokana na vigezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

- Uelewa wa wananchi wa haki ya kupata na kutoa habari ilivyo katika Katiba au kama itakavyofafanuliwa na sheria ya utekelezaji wa haki hiyo;

- Uongezekaji wa wasomaji wa magazeti, wasikilizaji wa redio, watazamaji wa televisheni na video na watumiaji wa intaneti, hasa vijijini;

- Uongezekaji wa Watanzania wanaomiliki magazeti, vituo vya redio, televisheni, intaneti na mashirika ya habari;

- Kudurusiwa kwa sheria zinazoathiri utendaji wa Sekta ya Habari na Utangazaji;

- Kutungwa kwa sheria moja ya vyombo vya habari na utangazaji;

- Kuongezeka kwa maudhui ya Kitanzania katika vyombo vya habari na utangazaji;

- Kupungua au kutoweka kwa malalamiko kuhusu uvunjaji wa maadili ya taaluma ya habari na ya jamii;

- Kuongezeka kwa wahitimu wa fani za habari na utangazaji na mawasiliano katika ngazi mbalimbali;

- Kuongezeka kwa wanahabari wenye mafunzo ya taaluma zingine kama uchumi, sheria, n.k.

- Kuongezeka kwa vyuo vinavyofundisha taaluma ya habari na utangazaji;

- Matangazo ya Redio Tanzania na Televisheni ya Taifa kuwafikia wananchi kote nchini.

*Mwisho*